

Mwongozo wa Maombi ya Leseni ya biashara kwa Wakopeshaji Binafsi wanaotoa Huduma Ndogo za Fedha bila Kupokea Amana

### **A. Maelezo ya Jumla**

1. Mwombaji anatakiwa awe amesajili jina la kibiashara kama mmiliki binafsi kwa mujibu wa sheria ya leseni za biashara
2. Jina la kibiashara la mwombaji linatakiwa liwe na maneno yafuatayo "Microfinance" "finance" "Financial Services" "Credit" au "Microcredit."
3. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya leseni ya shilingi 300,000 ambayo haitarudishwa.
4. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi isiyorudishwa kwa njia ya uhamisho wa moja kwa moja wa TISS kutoka benki zao kwenda Benki Kuu ya Tanzania.

Namba ya Akaunti ni: 9944713001

Jina la Akaunti ni: MFCs & FICOs Application and Licensing Fees

5. Mwombaji atahakikisha ana mtaji usiopungua shilingi milioni ishirini pale anapoanza biashara na wakati wote.
6. Sera ya Mikopo ioneshe mambo ya msingi yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Watoa Huduma Ndogo za Fedha Wasiopokea Amana.

### **B. Taarifa/Nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya Maombi ya Leseni**

1. Barua ya maombi kwenye fomu iliyoinishwa.
2. Hundi ya Benki au nyaraka nyingine zozote zinazokubalika na Benki kuthibitisha malipo ya ada.
3. Nakala iliyothibitishwa ya hati ya usajili wa jina la biashara
4. Uthibitisho wa chanzo na upatikanaji wa mtaji unaopendekezwa na mtoa huduma ndogo za fedha mtarajiwu.
5. Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya taaluma na utaalam vya Mtendaji Mkuu.
6. Nakala ya Taarifa za Fedha zilizokaguliwa hivi karibuni ikijumuisha mizania, taarifa ya mapato na mtiririko wa fedha wa mtoa huduma ndogo za fedha aliye na biashara tayari.
7. Nakala iliyothibitishwa ya hati ya Namba ya Mlipa Kodi (TIN).
8. Nakala iliyothibitishwa ya hati safi ya kodi kwa mwombaji,
9. Sera ya Mikopo
10. Tamko kwamba fedha itakayotumika kuwekeza haikupatikana kwa njia ya jinai au haihusiki na shughuli yoyote ya kijinai.

11.Uthibitisho wa uraia wa kila mwanahisa na mkurugenzi aliyependekezwa, Mtendaji Mtendaji Mkoo na mkopeshaji binafsi. Hii inajumuisha wasifu binafsi, picha mbili ndogo za hivi karibuni na mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:

- (i) Nakala ya kusafiria (passport) iliyothibitishwa, ambayo imebeba taarifa binafsi;
- (ii) Kitambulisho cha Taifa; au
- (iii) Cheti cha kuzaliwa

12.Dodoso liliøjazwa kikamili fu kwa ajili ya Mmiliki au Mtendaji Mkoo wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha Chini ya Daraja La 2 lilioko katika Jedwali la nne katika Kanuni

13.Taarifa za Mikopo kutoka Taasisi za Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo.

14.Taarifa za Mtu wa kuwasiliana naye zinazoonesha Jina lake, Anuani ya Posta, Namba ya Simu na Barua pepe

NB: Watoa Huduma ndogo za fedha walio katika Daraja la 2 linahusisha; Makampuni ya Kukopesha, Mashirika ya kifedha, makampuni ya kutoa mikopo midogo ya nyumba, Wakopeshaji binafsi na wakopeshaji wa kidijitali